**Learning by Ear 2009**

**Media & Information**

**Author: Hope Azeda**

**Redaktion: Ludger Schadomsky**

**Kisuaheli Translation:Eric Ponda**

**EPISODE 7**

| ***CHARACTERS*** | |
|---|---|
| **Announcer:** | **Male/female** |
| **"Young Junior"** | **Male, 15 years old** |
| **"Sister P."** | **Female, 16 years old** |
| **"Charlie"** | **Male, 18 years old** |
| **"Ezra":** | **Male, 22 years old. Brother to "Young Junior".** |
| **Director Press Council** | **Adult female** |

**INTRO**

Hujambo na karibu tena kwa makala yetu ya Learning By Ear tukizungumzia taaluma ya uandishi wa habari na Vyombo vya habari.Katika kipindi cha leo wanahabari wetu chipukizi wanajifunza mengi kuhusu baraza la waandishi wa habari. Wakati huo huo, Young J. anafaya mazoezi ya dakika za mwisho mwisho chumbani mwake kuhusu taaluma ya kuwa DJ.

Karibu tuandamane!

## SCENE ONE

**Young J's bedroom. Morning.**

| **SFX Morning sounds. Young J rehearsing his radio show.** |
| --- |

1. Young J: *Tumpa tumpapatu tumpa tutumpa pililililili tumpa tumpapapatu tumpa.*

**(Whistles the tumpa beat for some seconds and stops)**

**(In a fast radio presentation style)** Hujambo mpenzi msikilizaji mahali popote ulipo, ni wakati mwengine wa kipindi chako ikipendacho cha kumepambazuka.Unaendelea kusikiliza D.C FM, kituo kinachoporomosha miziki moto moto ya kizazi cha sasa, nikitumai kuwa ulikuwa na usiku mwema.Anayekukaribisha studioni si mwengine bali mtangazaji wako DJ Young J nikiwa tayari kukuporomosha vitu kama hivi ………

"Hoooo. Tumpa tumpapatu tumpa tutumpa pililililili tumpa tumpapapatu tumpa".

Naam…. ni asubuhi njema mepnzi msikilizaji na kama kawaida licha ya msongamano wa magari, najua wanafunzi wote sasa mumo mbioni kuelekea shuleni au vyuoni .Na kwa wafanyi biashara, wake wa waume mkiwa ndio mwanza munajiandaa kwa

shughuli za nawatakia biashara njema. Pia sitaki kuwasahau wakulima wanaotegemewa sana na taifa kwa chakula, nikitumai kuwa tayari mumenadaa majembe kuelekea shambani .Ujumbe wangu kwenu, msibanduke kwenye redio yenu ya Dot.Com.FM kwa burudani murua kabisa…..

***"…..Hoooo! Tumpa tumpapatu tumpa tutumpa pililililili tumpa".***

| SFX Door opening |
|---|

4. Ezra: Young J, .. nini kinachoendelea hapa?

5. Young J: ***"Hoooo…. Tumpa tumpapatu tumpa tutumpa pililililili tumpa"***

6. Ezra: Young J?

7. Young J: Ezra, Usinitatize na shughuli yangu! Niko hewani Bwana!. Nina fanya mazoezi ya kuwa mtangazaji kabla ya kuanzishwa kwa stesheni yetu. Au unasemaje?

8. Ezra: Naam.. naona unaendelea vyema sana .Nimekutana na vijana wengi wakikusikiliza huku wakitikisa vichwa. Je mumefikia wapi na mipango ya kukusanya fedha?

9. Young J: Tumepiga hatua kubwa sana. Katika ofisi zote tulikowasilisha mapendekezo yetu, wametupokea vyema na yapo matumaini makubwa. Baadhi yao kama vile mashirika yasiyo ya kiserikali na hata baadhi ya wafanyi biashara wametupa ahadi . Wengine wameahidi kutusaidia kwa hali na mali kwa mfano, duka kubwa la vyombo limeahidi kutupa vyombo vya studio. Na Isitoshe, unalijua lile duka la kuoka mikate, ***la Burgers & Burns*** karibu na kituo cha mabasi?, limeahidi kutupa chakula bila malipo endapo tutakubali kupeperusha matangazo yao ya biashara. Nakwambia,..kuku wao ni watamu wanaodondosha mate!.

10. Ezra: Hizo ni habari njema.

11. Young J: Hivi leo mchana ninakutana na Sister P na Charlie kujadiliana mipango ya kukusanya fedha zilizosalia.

12. Ezra: Yaonekana mwaendelea vyema. Lakini ni bora nimupe ushauri zaidi kuhusu redio ya jamii, na pia kuwashauri wenzako!.

13. Young J: Asante sana kaka.

14. Ezra: Suala mnalopasa kuzingatia zaidi ni kupata leseni. Katika siku za hivi punde, imekuwa vigumu kupata leseni na hilo huwa kikwazo kikubwa katika

kuanzisha kituo cha redio.Baadhi na stesheni zimechukua zaidi ya muda miaka 5 kupewe leseni

15. Young J: Usiniambie,…Ezra!. Kwanini inachukua muda hivyo?

16. Ezra: Kuna sababu nyingi tu.Mara nyingine utakuta ni kutokana na sheria zinazosimamia vyombo vya habari, maana wasimamizi huogopa athari zinazoweza kusababishwa na vituo vya utangazaji iwapo vitasimamiwa na watu wasiojali. Pia kuna suala la ufisadi. Umewahi kusikia kuhusu gazeti la Kangura na RTLM?

17. Young J: Bado. Ni kina nani hao?

18. Ezra: Ni mfano mzuri wa vyombo vya habari,yaani redio na gazeti vilivyotumiwa vibaya kuhubiri chuki na hatimaye kusababisha mauaji ya halaiki yaliyotokea nchini Rwanda. Zaidi ya watu milioni moja waliuawa katika muda wa siku 100 nchini humo. Kwa hivyo hatua ya serikali kuchelewesha otoaji wa leseni hizo, mara nyingine huwa ni kwasababu ya sheria na utaratibu wa kudumsha usalama wa taifa.

19. Young J: Sasa nimelewa unachomaanisha. Tusubiri mambo yatakavyokwenda.

20. Ezra: Suala jingine..!. huku mnapoendelea na mipango yenu, pia ni lazime mubuni maongozi bora ya utendaji kazi ,kwa mfano muda wa kuwa hewa kila siku na kuhakikisha mnavyo vipindi vizuri vya kutosha kwa muda huo wote wa matangazo.

21. Young J: Na bila shaka muziki mzuri wa kutosha.

22. Ezra: Kwa hakika muziki muzuri hufanya vipindi kuvutia.Pia mnapasa kuhakikisha mnatayarisha vindi vyenu wenyewe au kutafuta vipindi vya kutosha kutoka stesheni nyingine. Mbali na hayo mnahitajika kuandaa mijadal,vipindi vya mahojiano ya ana kwa ana kupitia njia ya simu na kadhalika.

23. Young J: (**Laughs).** Simu? Ezra yaani masomo yamekufanya usahau unakotoka.? Hebu niambie ni wangapi kijiji mwenu wanaweza kumudu gharama ya simu?

24. Ezra: Sawa unaweza kuzingatia yaliyo muhimu na jambo jingine, ili kuhakikisha wasikilizaji wanaendelea kusikiliza redio yenu ni lazima kuwahimiza watume maoni yao.

25. Young J: Ezra, hiyo ni kazi kubwa.

26. Ezra: Ndio, ni lazima hakuna kazi rahisi.Kama mumeamua kujitosa katika sekta lazime mujue munachokifanya. Pia munahitajika kufungua laini ya

simu ya uhariri, kujua habari munazotaka kuzifuatilia, muziki munaotaka kucheza, matangazo ya bishara na kadhalika.

27. Young J: Tosha ..tosha tutashiwa wazimu!.

**SCENE TWO**

**A class at the City Institute of Journalism**

| |
|---|
| **SFX: Noise of tables and chairs pushed on the floor, murmurs and footsteps of people leaving the room. The class has just ended and the students are excited.** |

30. Sister P: (**talking to someone some distance away)** Charlie ngoja kidogo usiende!. Kwanza tukubaliane tutafanya nini.

31. Charlie: (**Approaching)** Sawa!

32. Young J: Sasa tufanyeje baada ya haya yote?

33. Charlie: Twende tule chakula cha mchana,siendi darasa saa hivi.

34. Young J and Sister P: **Laugh**

35. Charlie: Mnacheka nini?

36. Sister P: Charlie, tunajua ni wakati wa chakula cha mchana, lakini kwanza unaweza kusahau mwito wako wa ***FF*** "Food First" yaani chakula kwanza ili tujadiliane

masuala ya bishara?.Young J, mueleze tulikuwa tukizungumzia nini.

36. Young J: Tulikuwa tukizungumzia mradi wetu wa Redio. Tunachopasa kukifanya kabla ya kuandaa harambee ya kukusanya pesa ya kufadhili mradi huo, mbali na kutafuta leseni.

37. Charlie: Samahani mawazo yangu yalikuwa mbali kabisa..!, sawa na mtu anayewinda Ndovu na kuishia kufuma Panya!. Kwa hivyo tufanyeje sasa?. Nani mwengine anaweza kutupa msaada au ushauri mbali na Ezra?

38. Sister P: Mwaonaje tukitafuta ushauri kutoka kwa vyombo vingine vya habari, kwa mfano baraza kuu linalosimamia shughli za vyombo habari?

39. Charlie: Unamaanisha nini ukisema hivyo, Sister P.?

40. Sister P: Baraza kuu la vyombo vya habari!. Hili linaweza kutusaidia kwa ufadhili na kupata leseni kwa urahisi au kutushauri ni wapi tunzweza kupata usaidizi.

41. Young J: Hiyo ni sawa na kumuomba mwenda uchi shati la kuvaa.

42. Charlie: Kwanini unasema hivyo Young J?.

43. Young J: Nafikiri baraza hili ni kama mwasisi wa vyombo vya habari,lakini lenyewe linakabiliwa na matatizo chungu nzima ya kufadhili shughuli zake.

44. Sister P: Unajuaje?, linaweza kutusaidia au kutushauri zaidi!.

45. Charlie: Pia nadhani ndilo linalohusika zaidi na masuala ya vyombo vya habari. Huwezi kuwa msimamizi katika mchezo usioujua.

46. Sister P: Kwanini tusijaribu?

47. Charlie: Kwanza tule kwanza kabla matumbo hayajaanza kunguruma!.

48. Sister P: Mimi pia nataka kula, Charlie!. Tunaweza kula njiani lakini ni muhimu twende ofisi za baraza kuu la vyombo vya habari tusikie ushauri wao, ili kufahamu vyema jukumu lake katika sekta hii.sawa?

**SCENE THREE**

**Outside the high press council offices, traffic noise.**

50. Sister P: Ofisi zote zimefungwa!

51. Charlie : Labda wamekwenda kula chakula cha mchana.

52. Young J: Na yule mama tuliyekutaka naye kwenye ngazi, labda ni mmoja wa mafia wa baraza hili. Twendeni tumuulize.

53. Sister P: Ndio huyo anaingia kwenye gari lake.

| | |
|---|---|
| **SFX:** | **A car door closing.** |

55. Sister P: Young J, anakimbia na kumsimamisha.

| | |
|---|---|
| **SFX:** | **A car starting.** |

57. Young J: **Shouting.** Samahani kidogo bibi.

| | |
|---|---|
| **SFX:** | **Car engine stopped.** |

59. Woman: **off mic.** Unazungumza na mimi?

60. All: Naam bibi!

| | |
|---|---|
| **SFX:** | **Fast foot steps as they run down the steps.** |

62. Young J: **Breathing fast.** Samahani kwa kukusumbua.

63. Woman: Sawa, Una shida gani?

64. Sister P: Tumekuja kutembelea ofisi hizi lakini tumepata zote zimefungwa. Je wewe ni mmoja wa maafisa katika baraza hili, na labda unaweza kutusaidia!

5. Woman: Munatoka wapi.?

66. Young J: Tunatoka chuo cha mafunzo ya uandishi wa habari hapa mjini.

67. Charlie: Tunatoka klabu ya Dot.Com.

68. Woman: Musinikanganye!. Sasa nimuamini nani?. Nijue munatoka chuo cha mafunzo ya uandishi wa habari au Klabu?

69. Sister P: Sisi ni wanachama wa DCC yaani ***Dot Com Club,*** na wakati huo huo ni wanafunzi katika chuo uandishi wa habari. Tuna mipango ya kuanzisha kituo cha utangazaji cha kijamii.

70. Woman: Ni vyema. Mimi ndie mkurugenzi katika baraza hili, kwa hivyo niwasaidie vipi?

71. Sister P: Baraza lenu linasaidia watu kupata leseni za vyombo vya habari?.

72. Young J: Na pia tungependa kujua iwapo baraza hili linasaidia watu kupata ufadhili. Kwa hivi sasa tumeweza kupata nusu ya fedha tunazohitahji na tunajaribu kukusanya kiasi kilichosalia.

73. Woman: Samahani baraza hili haliwezi kumsaidia.

74. Charlie: Nini?

75. Sister P: Kwa hivyo tufanyeje?

76. Woman: Baraza hili husimamia tu maadili na sheria katika sekta uandishi wa habari.

77. Young J: Nilimwambia hili ni baraza linalosimamia shughuli za uandishi wa habari ikiwa ni pamoja na kutetea haki za waandishi wa habari.

78. Charlie: Kwa hivyo nyiynyi ndio mnao kandamiza vyombo vya habari?.

79. Woman: La hasa. Labda katika baadhi ya mataifa, mabaraza haya mara nyingi yatumiwa na serikali kuvikandamiza nyombo na wandishi mbali na kuwatesa waandishi hao ambalo ni kosa kubwa sana. Jukumu kubwa la baraza hili ni kuhakikisha habari zote zinazotolewa na vyombo vya habari ni sahihi kuambatana na sheria za uandishi, maadili na kuhshimu haki za binadamu.Mbali na hayo kudumisha uhuru wa kutoa maoni kwa kuzingatia utaratibu na sheria zilizopo.

80. Charlie: Kwa hivyo hakuna msaada wowote tunaweza kupata kutoka kwa baraza katika mpango wetu wa kuanzisha kituo cha redio?

81. Woman: Baraza hili pia linajukumu la kutambua matatizo yanayowakumba waandishi wa habari na kujaribu kuboresha shughuli na mazingira wanamofanyia kazi kupitia mafunzo. Kwa hivyo labda nyinyi pia

kupitia juhudi zenu mutaweza kunufaika na mafunzo hayo.

82. Sister P: Na kuhusu suala la ufadhili?

83. Woman; (**laughs)** Pesa zetu zinatutosha tu kuendesha shughuli zetu hadi mwishoni mwa mwaka na hakuna fedha zaidi tunazopata kupitia ufadhili.Samahani sana kwa hilo!.

**SFX car engine starts**

**END EPISODE**

**OUTRO/NARRATOR**

Basi kama mulivyosikia, baraza linalo simamia shughuli za vyombo vya habari haliwezi kufadhili mradi wa wanahabari hawa chipukizi. Je ni vipi wataweza kukusanya kiasi cha Yuro 7,000 kununulia vifaa na kufungua ofisi.? Bila shaka umekuwa ukifuatilia vipindi vyetu kwa muda sasa. Hamu yetu kubwa hapa **Bonn** ni kujua, je unadhani lilikuwa wazo zuri kuanzisha kituo cha redio ya jamii?. Je unafkiri mradi huu utafaulu?. Na kwa maoni yako unadhani unaweza kuanzisha na kusimamia kituo cha redio au Gazeti? Tuma maoni yako kupitia mtanao wetu wa dw-world.de/l b e.Nikitumai utaungana nasi kwa makalal mengine ya LBE.Hadi wakati huo basi kwaheri kwa sasa.